GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXVII Nam. 6732 **5 Novemba, 2018** **Bei Shs. 2,500/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti

YALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali ya 2018 na mambo mengine yanayohusiana na hayo 264

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

Tangazo la Mswada

Nam. : Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali ya 2018

T A N G A Z O

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 28 Novemba, 2018 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
5 Novemba, 2018

(Dkt. ABDULHAMID Y. MZEE)
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

MSWADA
WA
MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajuulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali ya 2018 na itaanza kutumika mara tu baada ya kusainiwa na Rais.

Marekebisho ya Sheria mbalimbali.

2. Sheria zilizotajwa katika sehemu mbalimbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zinavyoelezwa katika sehemu husika .

SEHEMU YA PILI
MAREKEBISHO YA SHERIA YA JUMUIYA NAM. 6 YA 1995

Kusomwa.

3. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Jumuiya Nam. 6 ya 1995, katika Sheria hii itajulikana kama “Sheria Mama”.

Marekebisho ya kifungu cha 6.

4. Kifungu cha 6 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno “Shilingi Laki Mbili” na kuweka badala yake maneno “Shilingi Milioni Moja”.

Marekebisho ya kifungu cha 7.

5. Kifiungu cha 7 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu aya (b) kwa kufuta maneno “Shilingi Laki Mbili”na kuweka badala yake maneno “Shilingi Milioni Moja”.

Marekebisho ya kifungu cha 8.

6. Kifungu cha 8 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufuta maneno “Shilingi Laki Mbili” na kuweka badala yake maneno “Shilingi Milioni Moja”.

Kuongeza ya kifungu kipya cha 9A.

7. Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 9A mara tu baada ya kifungu cha 9 kama ifuatavyo:

Sifa za Mrajis.

“9A (1) Mtu atakuwa na sifa ya kuchaguliwa kama Mrajis akiwa :

(a) ni Mzanzibar;

(b) Mtumishi wa Umma;

(c) mwenye angalau Digirii ya kwanza katika Fani ya Utawala, Sheria, Sayansi ya Jamii au Fani nyengine zinahusiana na fani hizo katika Chuo kinachotambulika;

(d) awe na uzoefu wa kazi angalau miaka (9) katika fani zilizoainishwa katika aya (c) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hichi.

(2) Msaidizi Mrajis atakuwa na sifa sawa kama za Mrajis”

8. Kifungu cha 11 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuongeza aya mpya (c) mara tu baada ya aya (b) na kuzipa namba vifungu vyengine vilivyobakia kwa mpangilio: Marekebisho ya kifungu cha 11.

“(c) Kumbukumbu za Jumuiya zitajumuisha majina kamili na saini za wajumbe waanzilishi;”

9. Kifungu cha 13 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuongeza aya mpya (j) mara tu baada ya aya (i) kama ifuatavyo: Marekebisho ya kifungu cha 13.

“(j) Jumuiya inafanyakazi kinyume na utamaduni wa Zanzibar;”

10. Kifungu cha 15 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta neno “tatu” lilipo baina ya neno “ya” na “mwezi” na kuweka badala yake neno “mbili” Marekebisho ya kifungu cha 15.

11. Kifungu cha 19 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (3) kwa kufuta maneno “Shilingi Elfu Hamsini” na kuweka badala yake maneno “ Shilingi Laki Nne” Marekebisho ya kifungu cha 19.

12. Kifungu cha 24 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufuta maneno “Shilingi Elfu Hamsini” na badala yake kuweka maneno “ Shilingi Laki Nne” Marekebisho ya kifungu cha 24.

13. Kifungu cha 26 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (3) kwa kufuta maneno “Shilingi Elfu Hamsini” na kuweka badala yake maneno “ Shilingi Laki Nne” Marekebisho ya kifungu cha 26.

14. Kifungu cha 27 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufuta maneno “Shilingi Elfu Hamsini” na kuweka badala yake maneno “ Shilingi Laki Nne” Marekebisho ya kifungu cha 27.

15. Kifungu cha 29 cha Sheria Mama kinaerekebishwa katika kifungu kidogo cha (4) kwa kufuta maneno “Shilingi Elfu Hamsini” na kubadilisha kwa kuweka maneno “ Shilingi Laki Nne” Marekebisho ya kifungu cha 29.

16. Kifungu cha 40 cha Sheria Mama kama kifuatavyo: Marekebisho ya kifungu cha 40.

(a) katika kifungu cha (2) kufuta maneno “Shilingi Elfu Hamsini” na kuweka badala yake maneno “Shilingi Laki Nne”

(b) katika kifungu cha (5) kufuta maneno “Shilingi Elfu Hamsini” na kuweka badala yake maneno “Shilingi Laki Nne”

Marekebisho ya kifungu cha 45.

17. Kifungu cha 45 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kufuta maneno “Shilingi Elfu Hamsini” na kuweka badala yake maneno “Shilingi Laki Nne”

Kuongeza ya kifungu kipya cha 58A.

18. Sheria Mama imerekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 58A mara tu baada ya kifungu cha 58 kama ifuatavyo:

Kufungu cha 2(1)(c) Nam. 12 ya 2012.

“58A. Kifungu 2(1)(c) cha Sheria ya Usajili wa Biashara Nam. 12 ya 2012 kinafutwa Namba 12 ya 2012

SEHEMU YA TATU
MAREKEBISHO YA SHERIA YA UDHIBITI NA USAFIRISHAJI WA DAWA ZA KULEVYA NAM. 9 YA 2009

Kusomwa.

19. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Udhibiti na Usafirishaji wa Dawa za Kulevya Nam. 9 ya 2009, katika Shiria hii itajulikana kama “Sheria Mama”.

Marekebisho ya kifungu cha 4.

20. Kifungu cha 4 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa:

(a) Kuengeza mjumbe mpya katika orodha iliyopo katika aya (k) mara tu baada ya aya (j):

“(j) Waziri anayehusika na masuala ya Wanawake na Watoto.”

(b) Kuzipa herufi upya aya (k) hadi (q) kwa mpangilio wake.

Marekebisho ya kifungu cha 13.

21. Kifungu cha 13 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno “ au faini ya Shilingi Milioni Arobaini au adhabu zote mbili faini na kifungo”.

Kuongeza kifungu cha 13A.

22. Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 13A mara tu baada ya kifungu cha 13 kama ifuatavyo :

Katazo la kuchakata na umiliki wa kemikali bashirifu.

13A. Mtu yeyote amabaye kinyume na Sheria anachakata au anamiliki kemikali bashirifu anatenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini ya Shilingi Milioni Tano au kifungo cha kipindi cha miaka kumi na tano au vyote viwili faini na kifungo.

Marekebisho ya kifungu cha 15.

23. Kifungu cha 15 cha Sheria Mama kinarekebishwa:

(a) Katika kifungu kidogo cha (1):

(i) katika aya (b) kwa kubadilisha adhabu katika aya ndogo (i) kwa kufuta maneno “kifungo kisichopungua miaka kumi na tano na faini isiyopungua milioni ishirini na kuweka badalayake maneno “kifungo cha maisha”;

(ii) kuweka adhabu moja kwa moja katika aya (c) na itasomeka ifuatavyo:

“(c) anavuta, anafukiza, ananusa au vyenginevyo anatumia dawa za kulevya anatenda kosa na atakapotiwa hatiwani atatumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au faini isiyozidi Shilingi Milioni Mbili’

(b) Katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufuta rejea katika aya “(c)” katika orodha na rejea zinazoanzia aya (d) zitabaki kwa mpangilio wake.

Marekebisho ya kifungu cha 16.

24. Kifungu cha 16 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) Kufuta kifungu kidogo (1) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kifuatacho:

“(1) Mtu ambaye amekiuka sharti lolote la Sheria hii au kanuni au amri au ruhusa iliyotolewa chini ya Sheria hii anamiliki kiwango kidogo cha dawa za kulevya au atakuwa, bila kujali kitu chochote kilichopo katika Sehemu hii atakuwa anatenda kosa:”

(b) Kufuta neno “Tume” katika kifungu kidogo cha (2) linalojitokeza mwisho na kuweka badala yake neno “Waziri”

Marekebisho ya kifungu cha 19.

25. Kifungu cha 19 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) Kufuta maneno “ faini isiyopungua Shilingi Milioni Thelathini na “kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi” na kuweka badala yake maneno “kifungo cha maisha na faini isiyopungua Shilingi Bilioni Moja”.

(b) Kurekebisha kosa katika rejea “16” kusomeka “15”.

Marekebisho ya kifungu cha 47.

26. Kifungu cha 47 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (4) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (4) kifuatacho:

“(4) katika uendeshaji wa shauri chini Sheria hii, cheti cha uchungunguzi kilichoainishwa katika Sheria hii kutoka kwa

mchunguzi aliyeidhinishwa na kuweka saini yake kitakuwa ushahidi tosha kwa mambo yaliyoelezwa katika cheti kinachohusiana na dawa za kulevya".

Kuongeza kifungu kipya cha 60A.

27. Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 60A mara tu baada ya kifungu cha 60 kama ifuatavyo :

Kuzuia ,makosa usalama kwa kuweka amani na tabia njema

"60A.(1) Hakimu, baada ya mlalamikaji au kupokea taarifa kwa kiapo dhidi ya mtu yeyote aliyetuhumiwa kuwa anajihusisha katika makosa ya dawa za kulevya, anaweza kumtaka mtu aliyetuhumiwa kujitetea kuwa kwa nini asiamriwe kuweka dhamana kuhakikisha atakuwa na tabia njema kwa kipindi kisichozidi miaka miwili kama Hakimu atakavyoona inafaa.

(2) Katika kutekeleza uwezo wake aliyopewa Hakimu chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, masharti ya kifungu cha 60 hadi kifungu cha 74 vya Sheria ya Mwenendo wa Jinai yatatumika.

MADHUMINI NA SABABU

Madhumuni ya Mswada huu ni kufanya marekebisho katika Sheria Mbalimbali na kuweka badala yakemasharti yaliyobora ndani yake. Sheria zinazorekebishwa katika Mswada huu ni:

1. Sheria ya Jumuiya Nam. 6 ya 1995; na

2. Marekebisho ya Sheria ya Udhibiti na Usafirishaji wa Dawa za Kulevya Nam. 9 ya 2009.

Mswada huu umegawika katika Sehemu Tatu.

Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya awali ambapo ni jina fupi na kuanza kutumika kwa Sheria inayopendekezwa.

Sehemu Pili inahusiana na marekebisho ya Sheria ya Jumuiya, Nam.6 ya 1995. Katika Sehemuhi, marekebisho yanapendekezwa katika vifungu vya 6 , 7, 8, 19, 24, 26, 27, 29, 40 na 45 kwa kuongeza viwango vya adhabu , kuongeza kifungu cha 9A ambayo kinahusiana na sifa za Mrajis , kuongeza masharti ya maombi ya usajili wa Jumuiya katika kifungu cha 11(1) kwa kuongeza aya mpya (c) mara tu baada ya aya (b), kuongeza kifungu kipya cha 58A mara tu baada ya kifungu cha 58 ambacho kinapelekea kutwa kwa kifungu cha 2(1) (c) cha Sheria ya Usajili wa Biashara, Nam. 12 ya 2012.

Sehemu ya Tatu inahusiana na marekebisho ya Sheria ya Udhibiti na Usafirishaji wa Dawa za Kulevya Nam. 9 ya 2009. Katika sehemu hii, marekebisho yanayopendekezwa ni katika kifungu cha 4 kwa kuongeza mjumbe mmoja mpya wa Tume, katika kifungu cha 13, 15 na 19 kwa kuongeza viwango vya adhabu, katika kifungu cha 15(1) (c) kwa kupunguza adhabu za watumiaji, kuongeza kifungu kipya cha 13A ambacho kinaweka katazo la kuchakata na umiliki wa kemikali bashirifu na kuongeza kifungu kipya cha 60A ambacho kinaelezea kuzuia makosa, usalama kwa kuweka amani na tabia njema.

(SAID H. SAID)
Mwanasheria Mkuu
Zanzibar

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA UCHAPAJI WA SERIKALI ZANZIBAR - 2018